**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)**

**MKOA WA KIGOMA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU**

**KIKAO CHA CMT MWEZI OKTOBA 2021/2022 TAREHE 01/12/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA KASULU.**

***Imeandaliwa Na:***

**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji**

**Halmashauri ya Wilaya**

**S. L. P 97**

**KASULU.**

***www.kasuludc.go.tz***



CamScanner

**AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 01/12/2021.**

Agenda nane (8) ziliwasilishwa, wajumbe walipokea na kuridhia zijadiliwe kwenye kikao hicho Kama ifuatavyo

1.Kufungua Kikao.

2.Kuthibitisha Agenda za Kikao cha Tarehe 01/12/2021.

3.Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 20.10.2021.

4.Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 20.10.2021.

5. Taarifa ya Fedha Mapato na Matumizi Mwezi Octoba 2021. **:**

6.Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya UVIKO 19 kiasi cha shilingi 2,455,178,634.67 kwaajili ya ujenzi wa vymba vya madarsa 90,shule za Sekondari, posho za chanjo za Covid,ufuatiliaji wa tathimini, ujenzi wa nyumba ya watumishi,uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa kituo cha matibabu. hwk/fum/ag.na/29/2020/2021

7. Maombi ya kufuta hasara ya upotevu wa fedha shs 2,880,000.

8.Kufunga Kikao



CamScanner

**MUHTASARI WA KIKAO CHA CMT CHA MWEZI OKTOBA 2020/2021 TAREHE 01/12/2021.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURI WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1 | Emmanuel Ladislaus | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (mwenyekiti) |
| 2 | Michael N. Magesa | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala (Katibu) |
| 3 | Cosmas Msema | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 4 | Elias Mtakama | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 5 | Joseph Maiga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 6 | Gwamaka Panja | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7 | Jeconia J. N | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi. |
| 8 | Pelimina Msuta | kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. |
| 9 | Peter Kitogwe | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 10 | Bahati Onesmo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 11 | Mohamed Omary | Afisa Nyuki |
| 12 | Audax Kamugisha | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani |
| 13 | Robert Rwebangira | Kaimu Mganga Mkuu |
| 14 | Kilatu J. W | Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji. |
| 15 | Revocatus Mwombeki | Afisa Biashara |
| 16 | Almachius Njungani | Mratibu wa TASAF |
| 17 | Lessi J. Majala | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 18 | Chacha Matiko | Mhasibu wa Mapato |
| 19 | Atanas Msuta | Kaimu Mhandisi |
| 20 | Mikidard Mbaruku | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na ushirika |
| 21 | Vanica Ndelekwa | Mkuu wa Idara Usafi na mazingira |
| 22 | Emmanuel Ladislaus | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 23 | Peter Kitogwe | Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |

**SEKRETARIETI.**

1.Fiona E. Sephania.

2.Hildephonce Mchunguzi



CamScanner

**HWK/ CMT/AG. Na/23/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaomba kuchangia maoni yao na kutoa ushauri katika agenda zitakazojadiliwa.

**HWK/ CMT/AG.NA/24/2021/2022.KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 01.12.2021**

Agenda nane (8) ziliwasilishwa, wajumbe walipokea na kuridhia zijadiliwe kwenye kikao hicho Kama ifuatavyo

1.Kufungua Kikao.

2.Kuthibitisha Agenda za Kikao cha Tarehe 01/12/2021.

3.Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 20.10.2021.

4.Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 20.10.2021.

5. Taarifa ya Fedha Mapato na Matumizi Mwezi Octoba 2021. **:**

6.Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya UVIKO 19 kiasi cha shilingi 2,455,178,634.67 kwaajili ya ujenzi wa vymba vya madarsa 90,shule za Sekondari, posho za chanjo za Covid,ufuatiliaji wa tathimini, ujenzi wa nyumba ya watumishi,uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa kituo cha matibabu. hwk/fum/ag.na/29/2020/2021

7. Maombi ya kufuta hasara ya upotevu wa fedha shs 2,880,000.

8.Kufunga Kikao

**HWK/ CMT/AG.NA/25/2021/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 20.10.2021.**

Muhtasari wa tarehe 20.10.2021 ulisomwa, wajumbe wa kikao waliupokea na kuridhia ulisainiwa kuwa kumbukumbu ya kikao cha tarehe husika.

**HWK/CMT/AG.NA/26/20201/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 20.10.2021**

Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 20.10.2021 iliwasilishwa kwa wajumbe wa kikao kisha waliipokea na kujadili na kuazimia kama ifuatavyo;



CamScanner

Wajumbe walisistiza kuwa DAICO asimamie shamba la kilimo kwanza vizuri na mpango wa kufanya maboresho uliopitishwa kwenye kikao utekelezwe mapema ili shamba hilo lifanyiwe maboresho hii itatusaidia kukusanya mapato kwa msimu wa kilimo ujao.

**HWK/CMT/AG.NA/27/20201/2022 TAARIFA YA FEDHA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI OCTOBA 2021**

Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Mwezi Octoba 2021 iliwasilishwa na Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji kama ifutavyo-;

Halmashauri ya Wilaya Kasulu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imekadiria kukusanya jumla ya Tsh. 30,954,065,930.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya miradi ya maendeleo ambapo Tsh. 14,855,654,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara, Tshs.7,340,651,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa Idara zinazopokea ruzuku,Tshs 300,000,000.00 ni ada ya Huduma, Tshs 350,000,000.00 ni CHF na NHIF, Tshs 123,000,000.00 ni mchango wa ada za kidato cha tano na sita,Tshs.2,119,312,430.00 ni mapato ya vyanzo vya Halmashauri na Tsh.12,471,448,500 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mwezi Octoba 2021 mapato halisi ya Halmshauri ni kiasi cha Tsh.2,104,888,245.7 sawa na asilimia kumi na tisa (19) ya mapato kwa mwaka 2021/2022. Aidha mwezi Oktoba Halmashauri imefanya matumizi ya kiasi cha shilingi 1,593,418,599.4. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea, kushauri na kuazimia kuwa

Wajumbe walishauri kuwa kila Mkuu wa Idara ashiriki kikamilifu katikaukusanyaji mapato asiachiwe Mhasibu wa Mapato na timu ya kukusanya mapato.

Wajumbe wamesisitiza kuwa fedha zinapo pokelewa zifate utaratibu wa kifedha matangazo ya kupokea fedha yabandikwe

Wajumbe wameshauri kuwa Halamshauri inunue token nyingine kwa ajili ya Wahasibu ambao hawana na Afisa Manunuzi hiii tasaidia kurahisisha malipo mbalimbali kwa sasa tuna kwama kwa sababu wahasibu wote wanatumia token mbili tu.



CamScanner

**HWK/CMT/AG.NA/28/20201/2022 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA UVICO19 KIASI CHA SHILINGI 2,455,178,634.67 KWAAJILI YA UJENZI WA VYMBA VYA MADARSA 90,SHULE ZA SEKONDARI, POSHO ZA CHANJO ZA COVID,UFUATILIAJI WA TATHIMINI, UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI,UHAMASISHAJI WA CHANJO NA UJENZI WA KITUO CHA MATIBABU.**

Taarifa ya Halamashaumari kupokezi ya fedha za miradi ya UVICO19 kiasi cha shilingi 2,455,178,634.67 kwaajili ya ujenzi wa vymba vya madarsa 90,shule za sekondari, posho za chanjo za COVID,ufuatiliaji wa tathimini, ujenzi wa nyumba ya watumishi,uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa kituo cha matibabu iliwasilishwa kwnye kikao kama ifuatavyo-;

Fedha kiasi cha 1,800,000,000/= kwaajili ya ujenzi wavyumba vya madarasa 90 shule za Sekondari19,shilingi 27,428,121.54 posho za chanjo,shilingi 6,514,747.00 ufatiliaji wa tadhimini,shilingi 90,000,000.00 ujenzi wa nyumba ya Watumishi 3 in 1 shilingi 31,251,075.51 uhamasishaji wa chanjo na shilingi 500,000,000.00 ujenzi wa kituo cha matibabu. Baada yakuwasilisha wajumbe walipokea taarifa na kujadili yafuatayo

- Wajumbe walishuri kuwa fedha za ujenzi wa madarasa zisimamiwe vizuri na waliazimia mchakato wa manunuzi uanze mara moja kwani tukichelewa tutakawama katika utekelezaji vifaa vinaweza kupungua kwani ujenzi huu unafanyika Tanzania nzima, pia vifaa vya kiwandani vinunuliwa kwa pamoja kwa shule zote na sio kila shule kununua kwa mzabuni.

- Wajumbe wameazimia kuwa kila mkuu wa Idara apew shule ya kusimamia ujenzi ambaye atatoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi.

- Fedha zinasubiri utaratibu na maelekezo ufatiliaji ufanyike ili utekelezaji wa miradi uendelee.

- Wajumbe wamesisitiza kuwa kamati za manunuzi na kamati za ujenzi katika miradi hii zianze kufanya kazi na wakuu wa shule wasisistizwe na Afisa elimu kufata taratibu zote za matumizi ya fedha za serikali na utunzaji wa nyaraka za ujenzi kwaajili ya kumbukumbu. na Waheshimiwa Madiwani washirikishwe katika kila hatu ili uwepo uelewa wa pamoja katika kutekeleza miradi hii.



CamScanner

**HWK/CMT/AG.NA/29/20201/2022 MAOMBI YA KUFUTA HASARA YA UPOTEVU WA FEDHA SHS 2,880,000.**

Maombi ya kufuta hasara ya upotevu wa fedha kiasi cha Tsh.2,880,000 kwa mkusanya mapato (RS) wa Kurugongo bwana aliyevamiwa na majambazi akiwa anatekeleza majukumu yake kwenye kituo cha kazi na kupigwa risasi iliwasilishwa na Mweka Hazina baada ya hukumu kutolewa nakala ya hukumu hiyo iliwasilishwa kwa wajumbe. Baada ya uwasilisha hiyo wajumbe walipokea na kujadili baada ya kujiridhisha waliridhia kuwa hasara hiyo ifutwe ili mkusanya mapato huyo aendelee na kazi.

**HWK/CMT/AG.NA/30/2021/2022.KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa majadiliano mazuri, kisha aliwasisitiza wajumbe kuwa kila mtu afanyie kazi yale yalioagizwa na kikao. Baada ya kusema hayo, alifunga kikao saa 10:15 jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA:**

| | |
|---|---|
| MICHAEL N. MAGESA. | EMMANUEL R. LADISLAUS |
| Katibu | Mwenyekiti |
| Saini | Saini |
| Tarehe 1/12/2021 | Tarehe 01-12-2021 |